**RIPOTI FUPI YA ZIARA YA VIJANA WA AZANIAFRONT, FRONDENBERG, UJERUMANI, TAREHE 30/06/2016 – 20/07/2016**

Vijana 8 wa Azaniafront tulipata nafasi ya kuwakilisha vijana wenzetu ujerumani katika program inayoitwa youth exchange program iliyoanzishwa miaka kadhaa iliyopita na iliyotokana na urafiki kati ya kanisa letu la Azaniafront na Kanisa la kilutheri la Frondenberg, Ujerumani. Kwa kawaida program hii hufanyika kila mwaka mara moja kwa kupokezana. Mwaka wa 2016 mwezi wa sita tulipokea ugeni wa vijana wenzetu kutoka Frondenberg, Ujerumani.

Katika safari hii tulisindikizwa na Katibu wa kamati ya Uhusiano na habari Mzee Cuthbert Swai, pamoja na mtheolojia Mr. Joseph Mlaki ambaye alimwakilisha baba mchungaji Charles Mzinga.

Kipekee tunapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mungu kwamba tulisafiri salama na tulipokelewa vizuri na wenyeji wetu na kukamilisha yote kwa msaada wa Mungu.
Tuliianza safari tarehe 30/06/2016 alfajiri na kupokelewa siku hiyo hiyo saa mbili jioni kwenye uwanja wa kimataifa wa Dusseldoff ulioko takriban kilomita 119 kufikia mji wa wenyeji wetu wa Frondenberg.

Jumapili ya kwanza Tulikaribishwa kwa furaha usharikani hapo ibadani na kupata nafasi ya kujitambulisha na kukabidhi zawadi tulizoenda nazo kwa niaba ya uongozi wa kanisa letu AzaniaFront, na kuendelea kuwa na muda mzuri na wenyeji wetu. Na jumapili zote mbili zilizofuata tulisali kanisani hapo.

Tulipata nafasi ya kutembelea sehemu tofauti ikiwemo shule inayoitwa **Peter-Weiss-Gesamtschule** Iliyoko mji wa Unna kiasi cha kilomita 8 kwa gari kutoka frondenberg, na kupata nafasi ya kuingia madarasani na kuwa na mijadala kadhaa na wanafunzi wa shule hiyo.

Tulisafiri kuelekea Berlin mji mkuu wa ujerumani tarehe 5 Julai kwa treni ya aina ya ICE yenye mwendo wa kasi ya kilomita 300 kwa saa, na siku iliyofuata kupata nafasi ya kutembelea bunge la ujerumani. Tulitembezwa ndani ya Bunge huku tukipewa historia na maelekezo ya jinsi jengo la bunge hilo lilivyo, na jinsi bunge hilo linafanya kazi zake. Na baadae, tulikutana na Mbunge wa Frondenberg kwa takriban saa moja tukiwa na kipindi cha maswali na majibu, na akitueleza ni jinsi gani anafanya kazi zake kukidhi mahitaji ya wananchi.

Baada ya hapo tulipata pia fursa ya kuijua historia ya mji huo ikiwemo ni jinsi gani ulivyoathirika na vita vya kwanza na vya pili vya dunia na siku iliyo fuata tulirudi Frondenberg.

Tulipata fursa ya kuonana na Mayor wa mji wa Frondernberg na ilikuwa furaha sana kwake kutupokea kwa kukumbuka kwamba kila mara amekuwa akipokea wageni ofisini kwake kutoka Tanzania. Baada ya mazungumzo naye kwa muda wa saa moja na robo tuliweza kuimba, kitendo kilicho kuwa kivutio sana ofisini hapo na kufanya wafanyakazi kutoka maofisini kuja kutusikiliza.

Tunayo furaha pia kwamba tuliweza kumtembelea Mkuu wa jimbo la Kanisa la Unna na kupata nafasi ya kuongea naye mengi kuhusiana na kanisa na hasa kuhusu jinsi gani ambavyo kanisa linakosa uhai na hasa uwepo wa vijana kadri miaka inavyozidi kusogea. Tuliangalia changamoto hii sio kwa upande wao tu bali hata kwa upande wetu kwamba linakuwa ni tatizo linaloendelela kukua. Tulijifunza kwamba sisi tulio katika nafasi hii tunatumiaje mifano hiyo kuhakikisha kwamba hatufikii katika kiwango chao cha vijana kutokuwepo kanisani. Kwa mfano kutumia njia ya kuwekeza kwa vijana na wadogo zetu katika kuhakikisha si tu kuja kanisani bali hata kuwa na uadilifu katika yote na kumtumikia na kumtegemea Mungu.

Baadae tulisafiri kwa gari kuelekea kwenye ofisi za dayosisi Mji wa Dortmund ambako pia ndiko taasisi ya maswala ya ecumenical affairs na majukumu ya kimataifa ilipo, tukiongozwa na mwenyeji wetu Mr. Dirk Hillerkus. Siku hiyo tulipata mawasilisho au presentation iliyohusu mabadiliko ya hali ya hewa na mlinganisho wa adhari katika mabara tofauti duniani, kutoka kwa Dr. Judith, mtaalamu wa maswala ya Mabadiliko ya hali ya hewa katika taasisi hiyo. Baada ya hapo tulihusika katika mijadala kuhusiana na Mabadilio ya hali ya hewa (Climate Change and Climate Justice) ikiwemo vyanzo, athari pamoja na namna za kuweza kukabiliana na athari hizo tukihusisha namna ambavyo sisi kama kanisa tunaweza kuwa wa kwanza kuhakikisha mambo haya yanatekelezwa kuanzia ngazi ya familia.

Pamoja na hayo tulitembelela maonyesho ya Teknolojia mjini hapo Dortmund (DASA) na Tulijionea jinsi ambavyo teknolojia inachangia kurahisisha shughuli za maisha ya kawaida ya binadamu kama kilimo, ufugaji, ufumaji, usafiri n.k na kuona ni jinsi gani ambavyo wenzetu wameweza kutumia asilimia kubwa ya vitu vilivyokuwa vikitumika katika miaka ya nyuma kama mabaki ya usafiri wa treni, magari ya kivita n.k kama chanzo cha biashara

ya maonyesho na kutumia fursa hiyo kuelimisha jamii namna ambavyo ilikuwa katika miaka ya nyuma kulinganisha na sasa.

Siku za mwishoni mwa safari hii tulisafiri kuelekea mji wa Cologne kwa treni kwa umbali wa kilomita 140 toka Frondenberg.
Tulitembelea kanisa la Cologne (Cologne Cathedral) lenye uwezo wa kuingia watu 6,000 na kupata historia ya jinsi kanisa lilivyojengwa katika miaka ya 1200 na jinsi lilivyo pata uharibifu mkubwa kipindi cha vita vya kwanza na vya pili vya dunia. Tulipata pia nafasi ya kupanda juu kabisa ya kanisa hilo kutumia ngazi zenye idadi ya wingi wa mia tano, kwa muda wa nusu saa na kuweza kuona mji unavyooneka kwa juu.

Tulivutiwa sana na uhifadhi wa historia ya makanisa yote tuliyotembelea kule, kuanzia ujenzi hadi hali iliyopo sasa, na kupata changamoto ya kufikiri ni namna gani sisi tunaweza kujifunza uhifadhi huo na kusaidia watalii wa ndani na ne kufahamu historia ya kanisa letu.

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwako Baba Mchungaji, Baraza la wazee, uongozi wa kanisa pamoja na washarika kwa ujumla, kuruhusu nafasi hizi za vijana kuweza kushiriki katika uhusiano huu ulioko baina ya kanisa letu la Azaniafront na Frondenberg Ujerumani, kushiriki na kupata mafunzo ya yale yote ambayo vijana wanakutana nayo katika safari hizi. Na kwamba zinaleta manufaa ya kuongeza uelewa wa namna ya jinsi ambavyyo tunaweza kuleta mabadiliko yenye manufaa si tu usharikani, bali katika jamii kwa ujumla.

*/……..Imeandaliwa na Kijana Wilton Mtei, 24/07/2016*